



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## MATOKEO MUHIMU

# UTAFITI WA MAPATO NA MATUMIZI YA KAYA BINAFSI TANZANIA BARA, 2011/12



Ofisi ya Taifa ya Takwimu  
Wizara ya Fedha  
Dar es Salaam  
Novemba, 2013

## Utangulizi

Ripoti hii inatoa muhtasari wa matokeo muhimu ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi Tanzania Bara wa mwaka 2011/12. Uchambuzi wa Utafiti huu unalenga katika viashiria vya umaskini vilivyoainishwa katika misingi ya kitaifa na kimataifa kama vile Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2011/12-2015/16; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II, 2011/12-2015/16) na Malengo ya Milenia.

Kutokana na mabadiliko ya mbinu za Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi zilizotumika mwaka 2011/12 zikilinganishwa na zile za mwaka 2007 na mbinu za tafiti nyingine zilizotangulia, ripoti hii inatoa matokeo muhimu yatakayoweza kulinganishwa na matokeo ya tafiti zilizokwishaifanyika kuhusiana na viashiria vya umaskini usiokuwa wa kipato. Kutokana na maboresho mengi kufanyika katika mbinu za utafiti wa mwaka 2011/12, uchambuzi katika masuala ya viashiria vya umaskini unahitaji umakini wa hali ya juu. Aidha, ulinganishi wa viashiria vya umaskini utainishwa kwenye Ripoti Kuu ya Utafiti huu.

Utafiti wa mwaka 2011/12 umekusanya taarifa nyingi zikiwemo mpya zilizokusanywa kwa mara ya kwanza. Hali hii itawezesha kufanyika ulinganifu wa baadhi ya taarifa za utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi ya mwaka 2011/12 na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 kwa kuwa baadhi ya maswali yanafanana.

Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi Tanzania Bara wa mwaka 2011/12 umefanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kushirikina na Wizara ya Fedha-Kitengo cha Kuondoa Umaskini, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Kazi na Ajira, pamoja na Wizara ya Maji. Taasisi nyingine zinajumuisha; Benki Kuu ya Tanzania, Chuo cha Takwimu cha Afrika Mashariki, REPOA, ESRF, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (College of Arts and Social Sciences), UNICEF, WaterAid, UNFPA, HelpAge International na CIDA.

Aidha, msaada wa utaalamu uliowezesha kufanyika kwa utafiti huu ulitolewa na Benki ya Dunia, na Shirika la Kimataifa la Msaada la Uingereza (DfID).

Fedha za Utafiti huu zilitolewa na Serikali ya Tanzania, Wadau wa Maendeleo kupitia Mpango Kabambe wa Kuboresha na Kuimarisha Takwimu Tanzania na michango binafsi kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa, Umoja wa Ulaya na Shirika la Msaada la Kimataifa la Uingereza.

Taarifa za ziada kuhusu Matokeo ya Muhimu ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2011/12 zinapatikana katika Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Kivukoni Front, S.L.P 796, Dar es Salaam, Tanzania. Simu: +255 22 2122722/3; Nukushi: +255 22 2130852; Barua pepe: dg@nbs.go.tz.

## **Namna ya Kurejea Ripoti hii:**

Ofisi ya Taifa ya Takwimu Tanzania. 2013. *Utafiti wa Mapato na Matumizi wa Kaya Binafsi Mwaka, 2011/12: Matokeo Muhimu.*

## Utafiti wa Mapato na Matumizi Unakusudia:

“Kukusanya, kuandaa na kuchambua taarifa za mapato, matumizi na manunuzi ya kaya. Kutokana na taarifa hizi ni rahisi kutathmini sera mbalimbali za kijamii na uchumi pamoja na kutambua makundi ya watu yaliyoko kwenye mazingira hatarishi. Kama zilivyo tafiti nyingine zilizopita, Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2011/12 umelenga kutoa viashiria vitakavyosaidia kufuatilia na kutathmini maendeleo ya sekta mbalimbali zilizoainishwa kwenye Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II).”

## Muundo wa Sampuli

Utafiti umetumia sampuli wakilishi ya Tanzania Bara iliyohusisha maeneo 400 ya Kuhesabia Watu (maeneo 120 kutoka Dar es Salaam, maeneo 120 kutoka Maeneo Mengine ya Mjini na maeneo 160 kutoka Vijijini). Jumla ya kaya 10,400 zilichaguliwa kwa lengo la kuhojiwa katika utafiti huu, kati ya hizo ni kaya 10,186 zilikamilisha mahojiano. Sampuli iliyotumika ilitoka kwenye orodha ya maeneo ya kuhesabia watu iliyoandaliwa kwenye Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002. Mizania ya sampuli imetumika ili matokeo ya utafiti yaweze kuwakilisha watu wote wanoishi katika kaya binafsi. Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2011/12 unatoa taarifa ya watu Tanzania Bara kwa ujumla, Dar es Salaam pekee, Maeneo Mengine ya Mjini na Maeneo ya Vijijini.

Ripoti hii fupi inaonesha viwango vya umaskini kwa mwaka 2011/12. *Ulinganishaji wa mwelekeo wa umaskini na tafiti za Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi zilizopita utainishwa kwenye Ripoti Kuu, ikizingatiwa kuwa maboresho mengi ya mbinu za utafiti yamefanyika katika utafiti wa mwaka 2011/12 hivyo ulinganishi na uchambuzi wa taarifa za tafiti hizo unahitaji umakini.*

## Ukusanyaji wa Taarifa

Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2011/12 umekusanya taarifa nyingi zaidi kuliko tafiti nyingine za aina hii zilizowahi kufanyika nchini. Madodoso makuu manne yalitumika pamoja na shajara (kitabu cha kumbukumbu za kila siku) iliyotumika kuweka kumbukumbu ya taarifa za gharama, matumizi na mapato ya kaya katika kipindi cha siku 28 za utafiti. Wanakaya wenye umri kuanzia miaka 5 na zaidi walitumia shajara binafsi kuandika manunuzi na matumizi mbalimbali ya binafsi. Utafiti huu ulifanyika kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia mwezi Octoba 2011 hadi Octoba 2012.

Takwimu zinazokusanywa kutoka kwa watu na kaya zilihusu maeneo yafuatayo:

- Elimu na afya ya wanakaya;
- Manunuzi na matumizi ya kaya;
- Umiliki wa bidhaa za matumizi na mali;

- Makazi na vifaa vya ujenzi;
- Upatikanaji wa huduma na vifaa;
- Upatikanaji wa maji na usafi wa mazingira;
- Shughuli za kiuchumi na ajira;
- Utalii;
- Umiliki wa biashara zisizo za kilimo; na
- Shughuli za kilimo.

### Takwimu za Umaskini wa Kipato za Mwaka 2011/12

Mbinu ya upimaji wa umaskini kwa kuangalia **mahitaji ya msingi** hutumika kupima kiwango cha umaskini uliokithiri kwa Tanzania Bara. Njia hii inaonesha kiwango cha chini kabisa cha kipato anachohitaji mtu kwa ajili ya kukidhi mahitaji mbalimbali ya msingi. Hivyo, **kiwango cha chini cha umaskini wa mahitaji ya msingi ni kipato** kinachohitajika kukidhi mahitaji hayo.

**Kiwango cha umaskini wa chakula** ni gharama ya matumizi yote ya kaya ambayo yapo chini ya gharama wanayohitaji ili kukidhi mahitaji yao ya chakula. Kiwango hiki pia hujulikana kama kiwango cha umasikini ulio kithiri. Watu ambao wako chini ya kiwango hiki wanatambulika kuwa ni maskini kupindukia

#### **Sanduku Na. 1: JINSI YA KUTENGENEZA MSTARI WA UMASKINI**

Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi kwa Mwaka 2011/12 uliorodhesha manunuzi na matumizi yote ya kila siku kwa muda wa siku 28 kwa kaya zote zilizochaguliwa. Manunuzi na matumizi hayo yalijumuisha vyakula na vitu vingine vilivyopatikana (kununuliwa, kupewa au kuzalishwa) na kutumiwa na kaya. Utunzaji wa kumbukumbu za kila siku za taarifa za matumizi ya kaya haukujumuisha matumizi yasiyo ya moja kwa moja ya kaya kwa mfano ununuzi wa pembejeo za kilimo na ununuzi wa bidhaa kwa ajili ya biashara za kaya.


Kiwango cha umaskini wa chakula kwa thamani ya fedha ni matumizi ya kiwango cha chini cha aina mbalimbali za vyakula vyenye kufikia kiwango cha kilo kalori 2,200 zinazohitajika kwa mlo wa mtu maskini kwa siku katika mwezi kwa kuzingatia uwiano wa vyakula vilivyotumiwa na asilimia 10 hadi 50 ya watu wote. Gharama ya kununulia chakula cha mtu mmoja kwa siku bila kujali eneo analotoka ni shilingi 858. Gharama hii ilipatikana kwa kutafuta wastani wa aina 153 ya vyakula vyote vilivyotumiwa zaidi Tanzania Bara. Kiwango cha juu kidogo cha mahitaji ya msingi kinahusisha matumizi mengine yasiyo ya chakula kama vile nguo.

Kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi kwa Tanzania Bara ulifanyiwa marekebisha ya bei za vyakula vilivyotumiwa na kaya katika maeneo mbalimbali nchini kwa kipindi cha 2011/12. Mfano, bei za vyakula ni kubwa jijini Dar es Salaam ukilinganisha na Maeneo ya Vijijini, hivyo gharama ya kulipia mlo wa mtu mmoja kwa siku wenye kilo kalori 2,200 ni ya juu kwa jiji la Dar es Salaam.

Matokeo ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi kwa Tanzania Bara kwa Mwaka 2011/12 yanaonesha kuwa **Kiwango cha Umaskini wa Mahitaji ya Msingi kwa mtu mmoja kwa mwezi ni Shilingi za Tanzania 36,482/=** na **Kiwango cha Umaskini wa Chakula kwa mwezi kwa mtu mzima ni Shilingi za Tanzania 26,085/=**. Kwa kutumia takwimu hizi, matokeo yanaonesha kuwa zaidi ya robo (asilimia 28.2) ya watu wote waishio Tanzania Bara wako chini ya mstari wa kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi na asilimia 9.7 ya watu wote wapo chini ya mstari wa umaskini wa chakula.

**Jedwali 1: Kiwango cha Umaskini Tanzania Bara 2011/12 (Asilimia)**


	<b>Dar es Salaam</b>	<b>Maeneo Mengine ya Mijini</b>	<b>Maeneo ya Vijijini</b>	<b>Tanzania Bara</b>
Umaskini wa Mahitaji ya Msingi	4.2	21.7	33.3	28.2
Umaskini wa Chakula (Uliokithiri)	1.0	8.7	11.3	9.7



## Watu Maskini Wanaishi Maeneo Yapi?

Umaskini wa Mahitaji ya Msingi hutuwezesha kujua asilimia ya watu maskini wa kipato nchini. Pia huonesha mgawanyo wa watu maskini wa mahitaji ya msingi (chini ya mstari wa kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi) waishio nchini. Takwimu zinaonesha kuwa kuna tofauti kubwa ya umaskini wa mahitaji muhimu kati ya mijini na vijijini. Kwa upande mmoja, Kaya za jijini Dar es Salaam zina kiwango kidogo cha umaskini wa mahitaji ya msingi ukilinganisha na kaya zinazoishi katika Miji Mingine na Maeneo ya Vijijini. Ukijumuisha watu wote wenye umaskini wa mahitaji ya msingi nchini, inakadiriwa asilimia mbili (1.5) wanaishi jijini Dar es Salaam, asilimia 14.4 wanaishi Maeneo Mengine ya Mijini na asilimia 84.1 wanaishi Vijijini.

**Mchoro Na. 3: Mgawanyo wa Watu Wenye Umaskini wa Mahitaji ya Msingi kwa Maeneo, Tanzania Bara, 2011/12**



### **Mwenendo wa Umaskini toka Mwaka 2007 Hadi 2011/12**

Kiwango cha umaskini wa mahitaji ya msingi kulingana na utafiti wa mapato na matumizi ya kaya Binafsi wa mwaka 2011/12 kwa Tanzania Bara ni asilimia 28.2 ikilinganishwa na asilimia 33.6 kwa utafiti wa mwaka 2007. Hii inaweza kutafsiriwa kuwa umaskini umeshuka katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Hata hivyo, kutokana na maboresho ya mbinu za ukusanyaji na ukokotoaji wa viashiria vya umaskini yaliyofanyika katika utafiti wa mwaka 2011/12, viwango hivi vya umaskini haviwezi kulinganishwa moja kwa moja. Hata hivyo, mbinu za kitakwimu zilizotumika 2011/12 zimetumika kukokotoa viashiria vya 2007 kwa ajili ya kuweza kupima mwelekeo wa umaskini. Matokeo ya awali yanaonesha kupungua kwa kiwango cha umaskini kati ya 2007 na 2011/12. Upimaji wa mwenendo wa umaskini utaainishwa kwenye Ripoti Kuu ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi, 2011/12.

### **Kina cha Umaskini katika Utafiti wa Mwaka 2011/12**

Pamoja na kupima kiwango cha umaskini (wa kipato), ni vyema pia kupima na kujua wastani wa **Pengo la Umaskini**. Pengo la umaskini ni wastani wa upungufu wa matumizi yote ya mahitaji ya msingi yanayowezesha kuwatoa watu wenye umaskini ili wafikie mstari wa kupima kiwango cha umaskini. Ikiwa mtu yupo umbali mkubwa chini ya mstari unaopima kiwango cha umaskini, pengo lake la umaskini huwa kubwa. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa fahirisi ya wastani wa pengo la umaskini kwa watu waishio chini ya mstari wa masikini Tanzania Bara ni asilimia 6.7. Fahirisi ya Pengo la Umaskini kwa jiji la Dar es Salaam ni asilimia 0.8 na katika Maeneo Mengine ya Mjini ni asilimia 5.5. **Fahirisi ya Pengo la Umaskini** kwa Maeneo ya Vijijini ni asilimia 7.9. Tafsiri ya taarifa hizi ni kuwa watu wanaoishi kwenye kina kirefu cha umaskini wa kipato (wapo mbali chini ya mstari wa umaskini) wapo Vijijini.




**Jedwali 2: Fahirisi ya Pengo la Umaskini kwa Maeneo, Tanzania Bara, 2011/12 (Asilimia)**

	<b>Dar es Salaam</b>	<b>Maeneo Mengine ya Mijini</b>	<b>Maeneo ya Vijijini</b>	<b>Tanzania Bara</b>
Fahirisi za Pengo la Umaskini	0.8	5.5	7.9	6.7

Kipimo cha **Fahirisi ya Pengo la Umaskini** kinaweza kusaidia maafisa mipango na wasimamiaji wa sera mbalimbali za kijamii kujua ni kiasi gani cha fedha kitahitajika kufanikisha kuwatoa watu maskini katika hali hiyo ili wafikie mstari unaopima kiwango cha umaskini. Mahitaji haya ya fedha hupatikana kwa kuzidisha kiwango cha fahirisi ya pengo la umaskini nchini (0.067) na idadi ya watu waishio katika kaya binafsi (milioni 42.3) pamoja na kuzidisha na kiwango cha mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi (shilingi 36,482 kwa mwezi kwa mtu mmoja). Kwa kutumia taarifa za mwaka 2011/12, kiasi cha **Shilingi za Tanzania bilioni 103.3 kwa mwezi** (sawa na **fedha za Kimarekani milioni 64.6 kwa mwezi -US\$**) zitahitajika kuondoa umaskini wa mahitaji ya msingi kwa watu waishio chini ya mstari wa umaskini Tanzania Bara.

### **Muundo wa Kaya na Umaskini**

Tafiti mbalimbali zimeonesha kwamba kuna uhusiano wa karibu kati ya idadi ya watoto kwenye kaya na hali ya umaskini katika kaya. Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2011/12 unaonesha uwiano huu, ambapo hali ya umaskini imekuwa ikiongezeka kadiri idadi ya watoto (miaka 0 – 6) wanavyoongezeka katika kaya (Mchoro 4).

**Mchoro Na 4: Uhusiano wa Kiwango cha Umaskini kwa Idadi ya Watoto (miaka 0-6), Tanzania Bara, 2011/12 (Asilimia)**


Kiwango cha umaskini kinaongezeka kulingana na jinsi idadi ya watu katika kaya inavyoongezeka. Zaidi ya watu watatu kati ya watano (sawa na asilimia 61.9) ya watanzania masikini wanaishi kwenye kaya zenye idadi ya watu saba au zaidi (wastani wa idadi ya watu katika kaya ni watu watano).

**Jedwali 3: Umaskini na Muundo wa Kaya (Asilimia), 2011/12**

<b>Idadi</b>	<b>Kiwango cha umaskini</b>	<b>Mgawanyiko wa Watu maskini</b>
<b>Watoto miaka 0 - 6</b>		
Hakuna	19.8	17.2
Mtoto 1	23.2	22.6
Watoto 2	30.3	27.2
3 +	40.8	32.9
Jumla	28.2	100.0
<b>Watu katika kaya</b>		
1	2.1	0.1
2	9.1	1.3
3	12.9	4.1
4	16.4	7.2
5	23.1	11.5
6	28.0	13.8
7 +	38.9	61.9
<b>Jumla</b>	<b>28.2</b>	<b>100.0</b>

### Tofauti ya Kipato

Tofauti ya kipato ni jinsi ambavyo mgawanyo wa kipato usivyo sawa kati ya wanajamii. Kiasi cha matumizi kwa kila mwanakaya kinaweza kupima tofauti ya kipato katika jamii. Kwa kawaida, tofauti ya kipato hupimwa kwa kutumia kipimo cha tofauti ya kipato katika jamii. Kipimo cha Gini huanzia sifuri (0) kama hakuna tofauti ya kipato mpaka moja (1) kama kuna tofauti kubwa ya kipato.

Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2011/12 unaonesha kipimo cha Gini ni 0.34 kwa Tanzania Bara. Kwa kutumia kipimo cha Gini, tofauti ya kipato kwa mtu ni kikubwa zaidi kwenye miji mingine ukilinganisha na jiji la Dar es Salaam na maeneo ya vijijini. Kama watu wote wangepiganywa katika makundi matano yanayolingana kulingana na ukubwa wa matumizi yao kuanzia wa chini hadi wa juu, matumizi ya watu wa kundi la juu (matajiri sana) ni mara nne (4) ya matumizi ya kundi la chini (maskini sana) kwa Tanzania Bara.

**Jedwali 4: Kizio cha Gini na Uwiano wa Tabaka la Umaskini kwa Maeneo, 2011/12**


<b>Kipimo</b>	<b>Dar es Salaam</b>	<b>Maeneo Mengine ya Mijini</b>	<b>Maeneo ya Vijijini</b>	<b>Tanzania Bara</b>
Kizio cha Gini	0.35	0.37	0.29	0.34
Uwiano wa Tabaka la Juu na Tabaka la Chini la Maskini	4.1	4.7	3.5	4.1



## Viashiria vya Umaskini Visivyo vya Kipato

Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi 2011/12 unaonesha kwamba kwa wastani kaya ya Tanzania Bara ina watu watano. Takribani nusu ya wanakaya (asilimia 48) ni tegemezi (watoto wenye umri chini ya miaka 15 na wazee wenye umri wa miaka 65 na zaidi). Inakadiriwa kuwa robo (asilimia 24.7) ya kaya zinaongozwa na mkuu wa kaya mwanamke. Hii inaonesha kwamba, kulikuwa hakuna mabadiliko katika uwiano wa kaya zinazoongozwa na wanawake kati ya mwaka 2007 na 2011/12. Wakati uwiano huu unapungua kwa Dar es Salaam na maeneo mengine ya mijini, kuna ongezeko kidogo katika maeneo ya Vijijini. Aidha, maeneo mengine ya mijini yanaendelea kuwa na uwiano mkubwa wa kaya zenye mkuu wa kaya mwanamke.

**Mchoro Na 5: Asilimia ya Kaya Ambazo Mkuu wa Kaya ni Mwanamke kwa Eneo, Tanzania Bara, 2011/12.**




## Hali ya Makazi

Kumekuwa na ongezeko la uwiano wa kaya zinazoishi katika makazi yaliyo jengwa kwa vifaa vya kisasa – zege, mawe, saruji na vyuma. Asilimia 66 ya kaya mwaka 2011/12 zinaishi katika nyumba zenye paa za kisasa ukilinganisha na asilimia 55 ya kaya mwaka 2007. Vivyo hivyo, asilimia 73 ya kaya zinaishi kwenye nyumba zilizojengwa kwa kuta imara mwaka 2011/12 ukilinganisha na asilimia 33 za mwaka 2007. Kuta imara zinajumuisha kuta zilizojengwa kwa mawe, matofali ya saruji, au matofali ya kuchoma na paa za kisasa ni zile zilizojengwa kwa mabati.



**Mchoro Na 6: Asilimia ya Kaya Zenye Majengo Yaliyojengwa kwa Vifaa vya Kisasa, Tanzania Bara, 2011/12.**



Matokeo yameonesha kuwa mwaka 2011/12 asilimia 18 ya kaya za Tanzania Bara zinaishi katika nyumba zilizounganishwa na umeme wa gridi ya Taifa. Hili ni ongezeko la asilimia 6 ukilinganisha na matokeo ya mwaka 2007. Nyumba nyingi Maeneo Mengine ya Mjini zimeunganishwa katika umeme wa gridi ya Taifa kuliko Maeneo ya Vijijini. Utafiti huu pia umebaini asilimia 68 ya kaya zilizopo Dar es Salaam na asilimia 36 katika Maeneo Mengine ya Mjini zimeunganishwa katika gridi ya Taifa. Aidha, takribani asilimia 4 ya kaya za Maeneo ya Vijijini ndizo zilizounganishwa katika umeme wa gridi ya Taifa.

### Matumizi ya Nishati

Utafiti huu pia umeonesha kuwa mafuta ya taa yanatumika zaidi (asilimia 61) kwa kuangazia/mwanga kuliko vyanzo vingine Tanzania Bara. Matumizi ya mafuta ya taa kwa kuangazia katika Maeneo ya Vijijini ni asilimia 70, Maeneo ya Miji Mingine ni asilimia 55 na Dar es Salaam ni asilimia 23.

Matumizi ya umeme katika kaya kama nishati ya kupikia ni madogo (chini ya asilimia moja) ukilinganisha na matumizi ya kuni (asilimia 66). Kaya za Maeneo ya Vijijini hutumia kuni zaidi (asilimia 89) kuliko Maeneo ya Mijini (asilimia 30) na Dar es Salaam (asilimia 3).

### Umiliki wa Nyumba

Kuhusu umiliki wa nyumba, utafiti umebaini kuwa asilimia 76 ya kaya nchini zinamiliki nyumba wanazoishi. Uwiano huu ni mkubwa katika Maeneo ya Vijijini ambako asilimia 89 ya kaya zinamiliki nyumba wanazoishi. Umiliki wa nyumba ni asilimia 58 katika Maeneo Mengine ya Mijini na asilimia 37 katika jiji la Dar es Salaam.

### Umiliki wa Vyombo vya Usafiri na Mawasiliano.

Utafiti unaonesha kuwa asilimia 4 (angalia Jedwali Na. 6) ya kaya zinamiliki pikipiki, asilimia 55 zinamiliki redio, na katika asilimia 57 ya kaya zote kuna angalau mwanakaya mmoja anayemiliki simu ya mkononi. Umiliki wa simu za mkononi unatofautiana sana kwa maeneo. Wakati kiasi cha asilimia 78 ya kaya za Maeneo Mengine ya Mjini na asilimia 88 ya

kaya za Dar es Salaam zinamiliki angalau simu moja ya mkononi, ni asilimia 45 ya kaya za Maeneo ya Vijijini zinazomiliki angalau simu moja ya mkononi.

### **Elimu na Afya**

Utafiti umeonesha kuwa asilimia 20 ya Watanzania (Tanzania Bara) wenye umri wa miaka 15 au zaidi hawana elimu ambapo kwa mwaka 2007 ilikuwa ni asilimia 19. Mgawanyo kwa jinsi unaonesha kuwa wanaume wana elimu zaidi ya wanawake, asilimia 87 ya wanaume wenye umri wa zaidi ya miaka 15 wana elimu ukilinganisha na asilimia 76 ya wanawake.

Uandikishwaji katika shule za msingi kwa watoto wenye umri kati ya miaka 7 hadi 13 umeshuka na kufikia asilimia 78 kwa mwaka 2011/12 ukilinganisha na asilimia 84 katika mwaka 2007. Kiwango cha uandikishwaji katika shule za msingi bado ni kikubwa katika Maeneo Mengine ya Mjini ukilinganisha na Maeneo ya Vijijini. Kama ilivyokuwa katika mwaka 2007, uwiano wa wasichana wanaohudhuria (asilimia 77) shule za msingi unaendelea kuwa mkubwa kuliko wavulana (asilimia 71) katika Maeneo ya Vijijini.



Matokeo ya utafiti wa mwaka 2011/12 yanaonesha kuwa kulikuwa na ongezeko la wagonjwa au majeruhi waliotafuta huduma ya afya ukilinganisha na mwaka 2007. Asilimia 71 ya wagonjwa au majeruhi waliotafuta huduma hiyo wiki nne kabla ya utafiti ukilinganisha na asilimia 69 mwaka 2007



## Huduma ya Maji na Vyoo

Utafiti ulionesha kuwa, asilimia 69 ya kaya zinatumia vyanzo salama vya maji kwa kipindi vya mvua na asilimia 61 kipindi cha kiangazi. Vilevile umeonesha kuwa asilimia 84 ya kaya zipo umbali kiasi cha kilometa kutoka katika vyanzo salama kwa msimu wa mvua na asilimia 71 wakati wa kiangazi. Hata hivyo, ulinganifu wa matokeo ya mwaka 2007 hautawezekana kutokana na muundo wa swali kutotenganisha vipindi vya mvua na kiangazi kama ilivyofanyika katika utafiti wa mwaka 2011/12.



Matokeo ya utafiti pia yameonesha kuwa kaya nyingi Tanzania Bara zina huduma ya choo ingawaje kuna upungufu wa huduma hii kutoka asilimia 93 mwaka 2007 na kufikia asilimia 88 mwaka 2011/12. Upungufu huu kwa sehemu kubwa unatokana na kupungua kwa kaya zenye vyoo Maeneo ya Vijijini, kutoka asilimia 91 mwaka 2007 na kufikia asilimia 83 mwaka 2011/12. Kwa maeneo mengine kumekuwepo na ongezeko dogo la huduma ya choo katika kipindi husika.



## Shughuli za Kiuchumi, Umiliki wa Ardhi na Zana za Kilimo.

Watanzania walio wengi bado wanategemea kilimo kama chanzo chao kikuu cha ajira, ambapo asilimia 75 wanafanya shughuli za kilimo za kaya. Kilimo kimeendelea kuwa ni shughuli kuu katika Maeneo ya Vijijini na Maeneo Mengine ya Mjini ambapo asilimia 89 wapo vijijini na asilimia 44 Maeneo Mengine ya Mjini. Dar es Salaam, tofauti na maeneo mengine, shughuli kuu ya wakazi wake ni ajira binafsi zisizo za kilimo ambayo ni sawa na asilimia 38. Hata hivyo, matokeo haya ya utafiti hayawezi kulinganishwa na matokeo ya mwaka 2007 kutokana na mabadiliko ya muundo wa swali.



**Jedwali 5: Asilimia ya Mgawanyo wa Ajira kwa Shughuli Kuu za Kiuchumi kwa Maeneo, Tanzania Bara, 2011/12**

Shughuli	Eneo			
	Dar es Salaam	Miji Mingine	Vijijini	Tanzania Bara
Sheria, utawala na uongozi.	1.7	0.8	0.1	0.4
Wataalamu.	5	2.1	0.3	1
Fundi sanifu na utaalamu mwingine.	4.6	3.3	0.9	1.6
Karani.	2.6	0.7	0.1	0.4
Watoa huduma na wauzaji dukani.	15.7	5.6	0.9	3
Wataalamu wa kilimo na uvuvi.	0.7	0.6	0.7	0.7
Wahunzi na shughuli nyingine zinazohusiana.	8.1	2.8	0.5	1.6
Waungaji na waendesha mitambo na mashine.	8.8	2.8	0.3	1.4
Ajira zisizo na ujuzi.	5.1	2.7	0.7	1.5
Kilimo katika kaya.	4	43.9	88.5	73.6
Ajira binafsi zisizokuwa za kilimo.	37.8	28.3	5.7	12.3
Wasaidizi wa kaya wasiolipwa.	5.7	6.4	1.3	2.5
<b>Jumla.</b>	<b>100</b>	<b>100</b>	<b>100</b>	<b>100</b>

*Angalizo: Taarifa hizi ni za wanakaya wenye umri wa miaka 15 na zaidi.*

Upande wa umiliki wa ardhi, utafiti umeonesha kuwepo na ongezeko la wastani wa eneo la ardhi linalomilikiwa na kaya nchini kutoka ekari 5 mwaka 2007 na kufikia ekari 6 mwaka 2011/12. Hata hivyo, kumekuwepo na tofauti ya umiliki wa ardhi katika Maeneo ya Mjini na Vijijini. Kaya zilizopo Vijijini zinamiliki maeneo makubwa ya ardhi, wastani wa ekari 7 ukilinganisha na ekari 6 Dar es Salaam na ekari 5 Maeneo Mengine ya Mjini.

Utafiti huu pia umekusanya taarifa ya umiliki wa zana za uzalishaji unaohusiana na kilimo, mifugo na ardhi. Kiwango cha kaya zinazomiliki zana za kilimo za kisasa mfano matrika na jembe lake bado ni chache. Aidha, kiwango cha kaya zinazomiliki jembe la mkono ni kikubwa katika maeneo yote, ambapo kiwango cha umiliki Maeneo ya Vijijini kimeongezeka na kufikia asilimia 96.5 mwaka 2011/12 kutoka asilimia 87.6 mwaka 2007.



**Jedwali 6: Muhtasari wa Matokeo Muhimu ya Mwenendo wa Viashiria Visivyokuwa vya Kipato, Tanzania Bara, 1991/92, 2000/01, 2007 na 2011/12.**

<b>Kiashiria</b>	<b>1991/92</b>	<b>2000/01</b>	<b>2007</b>	<b>2011/12</b>
<b>Kaya na Hali ya Makazi</b>				
Wastani wa ukubwa wa kaya	5.7	4.9	4.8	5
Wastani wa asilimia ya wategemezi	40	42	43	48
Asilimia ya kaya zinazoongozwa na wanawake	18	23	25	25
Asilimia ya kaya zenye paa la kisasa	36	43	55	68
Asilimia ya kaya zenye kuta za kisasa	16	25	35	46
Wastani wa idadi ya watu kwa kulala chumba	2.6	2.4	2.2	2.7
Asilimia ya kaya zenye umeme	9	12	13	18
<b>Umiliki wa Vyombo vya Usafiri na Mawasiliano</b>				
Asilimia ya kaya zinazomiliki redio	37	52	66	55
Asilimia ya kaya zinazomiliki runinga	-	-	-	16
Asilimia ya kaya zinazomiliki pikipiki	0.7	0.9	1.5	4
Asilimia ya kaya zinazomiliki sim za mezani	1	1	1.1	1
Asilimia ya kaya zinazomiliki simu za mkononi	-	-	-	57
<b>Elimu, Afya, Maji Huduma za Vyoo</b>				
Asilimia ya wanaume wazima wenye elimu yoyote	83	83	83	87
Asilimia ya wanaweke wazima wenye elimu yoyote	68	67	71	76
Kiwango halisi cha Uandikishaji wanafunzi Shule za Msingi	-	59	84	78
Asilimia ya watoto wenye umri wa miaka 7-13 wanaosoma	57	61	86	82
Kiwango halisi cha Uandikishaji Shule za Sekondari (Kidato I – IV)	-	5	15	29
Asilimia ya watu wote wanaomuona mtoa huduma za afya	-	69	69	71
Asilimia ya kaya zinazo tumia vyanzo salama vya maji msimu wa mvua.	-	-	-	69*
Asilimia ya kaya zinazo tumia vyanzo salama vya maji msimu wa kiangazi.	46	55	52	61
Asilimia ya kaya zilizopo umbali wa kilometa moja kutoka chanzo kikuu cha maji msimu wa mvua	-	-	-	84
Asilimia ya kaya zilizopo umbali wa kilometa moja kutoka chanzo kikuu cha maji msimu wa kiangazi.	-	-	-	71
Asilimia ya kaya zenye kutumia choo cha aina yoyote.	93	93	93	88**
<b>Shughuli za Kiuchumi, Umiliki wa Ardhi na Zana za Kilimo-</b>				
Asilimia ya watu wazima wenye miaka 15 na zaidi wanaojishughulisha na kilimo kama shughuli yao kuu.	-	-	-	74
Wastani wa ekari za ardhi zinazomilikiwa na kaya maeneo ya vijijini.	-	6	5	7

\*Tafiti za HBS's zilizotangulia hazikutofautisha kati ya majira ya kiangazi na majira ya mvua.

\*\* Utafiti wa 2011/12 Wahojiwa walionyeshwa Kadi ya picha za aina mbalimbali za vyoo. Hii inaweza kuleta tofauti za matokeo ya matumizi ya vyoo.





## **Ofisi ya Taifa ya Takwimu**

### **DIRA**

**“Kuwa chanzo cha kuaminika katika kutoa takwimu rasmi na huduma za kitakwimu Tanzania”**

### **DHAMIRA**

**“Kutoa takwimu rasmi na huduma za kitakwimu zinazokidhi mahitaji ya watumiaji wa takwimu wa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kupanga mipango na kufanya maamuzi sahihi”**